# *YESU KRISTO YEYE YULE JANA, LEO, NA HATA MILELE*

. . .?. . .Watu wa Mungu wanaelewa ya kwamba Bwana Yesu amefufuka katika wafu, na anaishi miongoni mwa watu Wake leo. Vipi kama Yesu angesimama hapa amevaa suti hii, na viatu hivi? Angemwambia nini mwanamke huyu? Asingeweza kumponya; la hasha. Jambo pekee angaliweza kumfanyia lingekuwa, kusema, "Nilipokufa, miaka elfu moja mia tisa iliyopita, nilikuponya. Unaliamini?" Sasa, Yeye angejua alichokuwa akifanya, kile kilichokuwa maishani mwake. Angejua yote kumhusu, kama Baba angemwonyesha.

2 Ni wangapi wanaoamini hiyo ni kweli? Inua tu mkono wako, ili niweze kuona jinsi kusanyiko. . .Hilo ni jema. Natumaini wengine wenu mtaamini kabla haijaisha.

3 Sasa, kama Yesu alifufuka katika wafu na anaishi ndani ya kanisa leo, basi Yeye atafanya tu mambo aliyofanya wakati huo, kwa kuwa, "Ile. . ." Yeye alisema, "Mambo nifanyayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya; na makubwa kuliko haya. . ." Si makubwa zaidi katika ubora, maana isingewezekana. Alisimamisha maumbile, na kufufua wafu. "Lakini mengi kuliko haya mtafanya; kwa kuwa ninaenda kwa Baba Yangu." Kanisa limeenea ulimwenguni kote, ambapo Yeye angeweza tu kuwa mahali pamoja. "Mengi kuliko haya mtafanya; mambo nifanyayo ninyi nanyi mtayafanya." Hayo ndiyo mambo yenyewe aliyofanya. Na mengi zaidi, makubwa zaidi, kwa sababu itaenea kote ulimwenguni; nayo Injili ingeenda ulimwenguni kote, kuonyesha nguvu za Roho Mtakatifu, "na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

4 "Mungu ameweka kanisani, kwanza mitume, pili manabii, walimu, karama za uponyaji, kunena kwa lugha, kufasiri lugha; haya yote kwa ajili ya kuujenga mwili."

5 Nadhani, mama, ya kwamba mimi na wewe hatufahamiani. Sivyo? Hatufahamiani. Mimi, angalau, sikujui. Hunijui mimi? Vema. Sasa, hivi hutasimama hapa nje? Ili mimi, nikutambue tu kutoka kwa watu. Unaona, mna roho kila mahali, juu, na kote; na kila mwanadamu ni roho. Sasa, itanibidi kuzungumza nawe, kama tu vile Bwana wetu alivyozungumza na yule mwanamke kisimani, vile vile tu. Mnaona? Ninii tu. . .Nafikiri, bila shaka, mimi mwenyewe, ya kwamba Yeye alikuwa na sa—sababu ya kufanya hivyo, maana katika kufanya hivyo, Yeye aliwasiliana na roho yake. Mliona yale aliyosema? "Nipe maji ninywe," ili tu kuvutia usikivu wake.

Naye akasema, “Vema, kisima ni kirefu Nawe una. . .” kwanza, alisema, “Vipi, kwa nini, vipi hii? Vema, ninyi Wayahudi hamna uhusiano wowote na Wasamaria.”

Naye akasema, “Lakini kama ungalijua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe; ningekuletea Maji ambayo hukuja hapa kuteka.”

Akasema, “Kisima ni kirefu,” na kadhalika.

Ndipo alipopata kujua shida yake ilikuwa wapi, akasema, “Nenda, kamwite mumeo.” Unaona? Yeye alifanya nini? Akashika roho yake.

6 Nayo roho yako ni picha moja thabiti ya jinsi maisha yako yamekuwa. Ndipo alipoishika hiyo roho, na kuishi katika maisha hayo ya roho, iliingia tu, ikarudi kwenye chochote Mungu alichomtaka ajue.

7 Sasa, hivyo ndivyo anavyofanya usiku wa leo. Ninaona, nikiangalia huko kwenye kusanyiko, naona kungekuwako, loo, watu mia kadhaa hapa, kila mmoja wao ni roho. Kila mmoja wao, sasa hivi, akivuta.

8 Nawe unajua kwamba jambo fulani linaendelea. Siwezi kujua ni nini, lakini kuna jambo fulani linaloendelea. Mara ulipokuja hapa, Kitu fulani kilikuja juu yako. Je, hiyo ni kweli? Vema kile hasa unachoona kwenye ile picha, hivyo ndivyo tu unavyojisikia sasa. Hiyo ni kweli kabisa. Sasa, sijui hata jambo moja lako. Mungu anajua hata sijawahi kukuona, wala chochote kukuhusu, maishani mwangu. Lakini Yeye anakujua. Ananijua.

9 Sasa, kama mimi ni mtumishi Wake, nami nimeshuhudia kweli, basi angeweza, kama alitaka, kunifunulia jambo lingine ambalo lingekusaidia. Kama wewe ni—kama wewe ni mgonjwa, ningejua hilo. Kama huna uhusiano mzuri na Mungu, ningejua hilo, kama Yeye angeniambia. Sijui, lakini Yeye anajua. Sasa, ninamtumainia Yeye aniambie.

10 Na kama angefanya hivyo, baada ya sisi kuona jambo hilo dhahiri sana, na wewe ni. . . Jambo la kwanza, Neno lilisema ya kwamba angefanya hivyo, sivyo? Angekuwa vivyo hivyo. Halafu jambo la pili ni kwamba, umesimama hapa na unafahamu kwamba uko Uweponi mwa Kitu fulani mbali na ndugu yako. Hiyo ni kweli? Na jambo la tatu ni kwamba umeiona picha Yake. Na sasa jambo lingine lingekuwa, kama Yeye angeninii, baada ya mambo haya yote, kama angekuja na kuthibitisha mambo hayo kuwa ni kweli. Hiyo ni kweli?

11 Unaamini, kwa msaada wa Mungu, ninaweza kufanya jambo hili? Na kama angelifanya, kusingekuwako na kivuli cha shaka tena? Basi, kama ningekwambia hilo, kwa Roho Wake, halafu kama ningekwambia jambo lingine, ungeniamini basi, sivyo?

12 Vema, hivyo ndivyo alivyoniambia wakati aliposema mambo haya: Nilitumwa kuwaombea wagonjwa. Na kama ningewafanya

waamini na wawe waaminifu, hakuna chochote kingesimama mbele ya hayo maombi.

Vema, nikasema, "Hawataniamini. Sina elimu."

Akasema, "Kama vile nabii, Musa, alivyopewa ishara kuthibitisha, vivyo hivyo nawe umepewa." Basi akaniambia hivyo.

Nami nikasema, "Hilo ndilo lililonileta hapa, nililokuwa nikiombea."

13 Akasema . . . Kisha akaninukulia Maandiko. Ndipo nikaona Yeye alikuwa sahihi Kimaandiko; nami nikaukubali. Basi tangu wakati huo, liko katika kila taifa chini ya mbingu, nijuavyo mimi. Yeye si ni wa ajabu?

14 Wewe hutoki katika mji huu. Umekuja huku, ukiendesha gari kutoka mbali. Unaishi katika jiji kubwa, nalo jiji hilo liko karibu na mto mkubwa. Ni Mto Mississippi, unaopitia karibu na mji huo, na kuna chemchemi iliyo na samaki inayobubujisha maji, na upande huo mwingine kuna saa. Ninaamini iko juu ya jengo fulani. Ni, unaishi St. Louis. Je, hiyo ni kweli? Imeniacha sasa. Hebu kidogo, iweni tu katika maombi. Je, hiyo ni kweli? U—una . . . shida yako iko ubavuni mwako. Una vivimbe mbavuni mwako. Hiyo si ni kweli? Ninaona uchunguzi wake u—ubavuni.

15 Na hivi, mtu fulani hakuja hapa pamoja nawe? Una marafiki wawili waliokuja pamoja nawe, nao ni wanawake wawili. Na mwanamke mmoja anaugua u—ugonjwa wa tumbo na ugonjwa wa kike. Hiyo si ni kweli? Na mwingine ana ki—ki—ki—kitu fulani kooni mwake. Ni—ni tezi kooni mwake, na ana ugonjwa wa moyo. Hiyo ni kweli? Hiyo ni kweli, inua mkono wako. Mungu akubariki.

16 Hao wanawake wameketi moja kwa moja huko nje. Simameni, enyi kina mama. Simameni, nyote wawili, huko nje. Simameni kwa miguu yenu kusudi watu waweze kuona. Basi simameni tu, msiogope. Naam, mama. Nyote wawili nendeni nyumbani, mmeponywa. Nawe pia. Yesu Kristo huondoa yote. Mungu awabariki.

17 Mwamini tu Mungu. Mungu atakufanyia mambo makuu, kama tu utaamini. Lakini lazima uamini kwamba Yeye yuko, kwa kuwa wale wamjiao hawana budi kuamini kwamba Yeye yuko, na ni Mpaji thawabu wale wamtafutao kwa bidii. Mwaminini Yeye, naye Mungu atalithibitisha Neno Lake kila wakati, kwa ishara na maajabu yakifuata. Sasa, iweni na kicho.

18 Jambo fulani limetukia mumu humu ndani. Hivi huna ugonjwa wa kibofu nyongo, uliyeketi hapo, mama? Hiyo si ni kweli? Uliponywa tu, wakati uo huo. Mungu alikuponya. Simama kwa miguu yako, na uukubali kama kumkiri Yesu Kristo. Mungu alikuponya, wakati huo. Umekuwa na tumbo chungu na kadhalika na hisia ya moto mle ndani. Nilimwona

mtu akichunguza, akalisukuma ndani, lilikuwa linauma, nawe ukaruka walipofanya hivyo. Umeponywa sasa. Mungu akubariki. Uh-huh.

19 Huyo mwungwana aliyeketi karibu nawe hapo, aliye na shida ya mgongo, anaweza kuponywa pia, kama tu ataukubali. Utaukubali, pia, bwana? Sivyo? Simama kwa miguu yako na kuukubali ninii wako. . . Mgongo wako ni mzima sasa. Unaweza kwenda nyumbani. Yesu Kristo anakufanya mzima.

20 Mwaminini Mungu. Msitie na shaka. Aminini ya kwamba mambo yote yanawezekana. Mnaamini hilo? Ninaamini ya kwamba lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa. Hivi huamini hivyo? Unawazia nini, huko juu? Unawazia nini, hapa kwenye vipandio? Unaamini kwa moyo wako wote? Chochote utakachomwomba Mungu, Mungu atakupa.

21 Vema, mlete huyo mama. Mwacheni tu aketi chini hapo, iwapo hawezi kutembea vizuri sana. Simama papo hapo ulipo, ama, njoo hapa, dada. Unakuja, nami ninataka uje kwa uchaji, ukiamini. Ninaona umelemaa. Ninataka unitazame. Ninataka uniamini. Kama ningeweza kukuponya, mama, ningekuponya, bali siwezi kukuponya, haiwezekani kwangu kukuponya. Lakini wakati huu, Mungu anaweza kufanya hivyo.

22 Wewe uliyemleta, unaamini? Kama vile nabii Eliya alivyosema, “Kama nisingemheshimu Yehoshafati, nisingeangalia.” Kama Petro alivyosema, kwenye lango liitwalo Zuri, “Tutazame sisi.” Sio kuwaangalia kama chochote, bali kuangalia kuwa makini, kuzingatia.

23 Hatufahamiani, mama. Sikujui. Kama nimewahi kukuona. . . Ni—ninaona umati mkubwa umesimama mbele yako, sasa hivi. Umekuwa kwenye mkutano mahali fulani hapo kabla. Na mahali ulipokuwa, kuna sehemu kubwa ya ardhi tambarare. Ina—ina mipungate mingi juu yake. U—unatoka Arizona; maana kuna mipungate mikubwa mno inayosimama moja kwa moja mbele yangu sasa. Hakuna mahali pengine ulimwenguni ambapo hukulia, ila kule. Hiyo si ni kweli? Unatoka Arizona. Na unaugua ninii. . . ni kansa. Nayo hiyo kansa iko kwenye nyonga yako kisha ikaingia kwenye uti wako wa mgongo. Madaktari hawawezi kufanya lolote kuihusu. Hiyo ni kweli? Unaamini Yeye atakuponya sasa? Njoo hapa.

24 Je, yawezekana unamfahamu Hattie Waldrop, huko Phoenix? Alikufia kwenye mstari wa maombi kwa kansa ya moyo, miaka saba iliyopita. Anaishi Phoenix siku hizi, mzima na mwenye afya. Alikuwa amefia kwenye mstari wa maombi kwa saa kadhaa, kabla hawajamwingiza ndani. Kansa iliyokuwa imepitia kwenye moyo wake, utumbo mpana na ini. Daktari wake. . . Naamini anwani yake iko kwenye kile kitabu walicho nacho wale wasichana. Mungu, aliyemponya, anaweza kukuponya. Hiyo ni kweli? Hivi unaenda nyumbani, ukiamini?

25 Nitaomba, Mungu na akubariki. Huku sote tukimwombea mwanamke huyu. Mungu asipomsaidia, atakufa katika mabadiliko machache ya mwezi. Hebu, tuombe tu.

26 Baba yetu wa Mbinguni, wakati maskini mama huyu akisimama hapa, kwa kuwa giza linaingia mahali aliposimama, huku tukijua ya kwamba nguvu hizi za mauti zimekuja juu yake. Nao watumishi Wako, madaktari, wamefanya yote wawezayo kufanya kusaidia, wala hakuna kinachoweza kufanywa katika uwezo wao. Naye huyu mwanamke amekuja kuponywa. Naye Shetani amekusudia kuuchukua uhai wake; anaula mwili wake; mwili wake upatikanao na mauti unamwacha. Lakini Wewe, Ee Mungu, Wewe ni Mungu wa Milele na Milele. Basi yasikie maombi ya mtumishi Wako asiyefaa, Bwana, na ulithibitishe Neno. Na ujalie Malaika aliyenena nami usiku huo, na hata akamtaja huyu pepo, kansa, jalia aje na kuukaribia ugonjwa huu wakati huu, na kumkemea adui huyu mbaya sana.

27 Ewe pepo unayeitwa kansa, ambaye umeyatesa maisha ya mwanamke huyu ili kumwua, ninakuapisha, kwa Yesu Kristo Mwana wa Mungu, kwamba umwachilie na kumwacha aende.

Basi Mungu wa Mbinguni na ambariki, na Yesu Kristo amponye. Amina.

28 Sasa, angalia huku tena, mama. Kama Mungu alijua kilichokuwa maishani mwako . . . Sijui sasa, yale Yeye aliyokwambia. Lakini je, hayo yalikuwa ni kweli? Yale—yale uliyoambiwa nilipokuwa katika ono, yalikuwa ni kweli? Yale aliyokwambia, yaliyotukia, na chochote kile kilichokuwa maishani, hayo yalikuwa ni kweli? Sasa, unaamini ya kwamba ninasema kweli? Basi, miaka elfu moja mia tisa iliyopita, Yesu Kristo alikuponya bila shaka yoyote, Maandiko yanasema hivyo. Je, sasa unaukubali kwa misingi hiyo, na kukataa kujua jambo lingine lolote kuhusu kansa ama chochote kile; unajua Yesu pekee ndiye anayekuponya? Je, hivyo ndivyo unavyotoka hapa kwenda kushuhudia?

29 Angalia, kulikuwa na wenye ukoma waliolala langoni. Wakasema, "Kwa nini tuketi hapa hata tufe?" Kama waliketi pale, walikufa; kama waliingia mjini, walikufa. Nao walikuwa na nafasi moja tu, hiyo ilikuwa ni kushuka kwenda kwenye kambi ya adui. Kisha kasema, "Wakituokoa, tutaishi; bali wakituua, tutakufa."

30 Vema, umeketi mahali pale pale, ila hujaalikwa kwenye kambi ya adui, umealikwa kwa Yesu, Ambaye anakukubali sasa hivi. Je, unakuja? Unaukubali, sasa hivi? Basi, katika Jina la Yesu Kristo, ondoka jukwaani, upate afya. Usiondoke kwa siku chache, na utushuhudie, kisha uje jukwaani, utuonyeshe yale Mungu amefanya. Mungu akubariki. Dada, wewe nenda moja kwa moja pamoja naye, na Mungu akubariki.

31 Vema, mlete huyo kijana mwanamume. Kijana, unaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu? Basi, kama mimi ni mtumishi wa Mungu, na upako Wake uko juu yangu, hakuna kitu ulimwenguni ambacho kingeweza kufichwa maishani mwako sasa hivi. Kukuponya, nisingeweza. Mimi si mponyaji. Mimi siye Mponyaji; Yeye ndiye Mponyaji. Lakini, unaamini ya kwamba Yeye ni Mfunuzi wa siri za moyo, na humfunulia nabii Wake mambo anayotaka wajue? Nitazame mimi kwa dakika moja tu.

32 Wewe si mgonjwa. Unakuja hapa juu kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli? Umekuwa ukiutafuta, kwa muda mrefu. Hiyo ni kweli? Kweli unamtaka Roho Mtakatifu? Njoo hapa.

33 Mungu, mbariki mvulana huyu na umjaze na Roho Mtakatifu; na jalia jua lisichomoze mara nyingi mpaka amejazwa na Roho Mtakatifu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Nenda, nawe utaupokea sasa, ndugu. Nenda ukishangilia, ukimshukuru Mungu kwa ajili yake.

34 Na tuseme, “Amina.” Sijasisimkwa hata kidogo, lakini Roho wa Mungu anatulia juu ya chumba hiki, hata jambo lolote lingeweza kutukia. “Kwa nini tuketi hapa hata tufe?” Hebu tuamke na kufanya jambo fulani kulihusu.

35 Unataka kuponywa ugonjwa huo wa kibofu, uliyeketi hapo, bwana? Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Unaamini Yeye atafanya hivyo? Mungu akubariki. Inua mkono wako, useme, “Ninaukubali katika Jina la Yesu.” Unaamini, Mungu atakuponya; kama unaamini, na unataka kuponywa, Mungu atakuponya bila shaka. Mungu akubariki. Hiyo ndiyo njia. Nenda nyumbani ukapone sasa.

36 Una kivimbe kidogo shingoni mwako, sivyo, dada? Bila shaka, macho yako yana shida, pia. Unataka kupona? Simama kwa miguu yako na ukubali uponyaji wako basi, katika Jina la Yesu Kristo, nenda nyumbani. Kivimbe hicho kimetoka shingoni mwako sasa. Unaweza kwenda nyumbani na uwe mzima.

Huhitaji kadi yako ya maombi. Unahitaji imani katika Mungu. Mwaminini Mungu, ninyi nyote; mtaponywa.

37 U hali gani, mama? Unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini ya kwamba Mungu alinituma kukusaidia? Unaamini. Loo, umekuja hapa kwa ajili ya mtoto huyu mchanga. Si kwa ajili yako, ni kwa ajili ya huyu mtoto mchanga. Una wasiwasi mno; hiyo ni kwa sababu. . .kwa ajili ya huyu mtoto mchanga. Vema, maskini mtoto huyo mchanga mpendwa. Ninakutaka unitazame kwa dakika moja tu. Ninakutaka uamini.

38 Unajua, dada, nina mtoto mchanga aliyeketi papo hapo. Na kama ningeweza kufanya lolote, kama mtoto wangu mchanga

alikuwa ni mgonjwa, ningefanya lolote niwezalo, kumshawishi Mungu amponye.

39 Na jambo pekee ninaloweza kufanya hapa kumsaidia mtoto wako mchanga ni, labda, kama Mungu atanifunulia jambo fulani, itakayosaidia imani yako, kujua mtoto huyo ana shida gani. Unajua simjui mtoto huyo, sivyo? Sijawahi kukuona, wala mtoto mchanga, ama hakuna njia ya kujua lolote kukuhusu.

40 Lakini, unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? [Huyo dada anasema, "Ninaamini."—Mh.] Unaamini. Mungu akubariki. Unapotoa tamshi la namna hiyo la kukiri imani yako, linampendeza Mungu.

41 Ulimleta mtoto huyo kutoka mbali sana hapa. Unatoka katika nchi iliyo na vilima na miti mingi migumu juu yake: Missouri. Hiyo ni kweli? Mtoto wako mchanga: hawajui ana shida gani; daktari hawezi kuamua; baadhi yao wanasema ni kifafa; na wengine wanasema ana—ana—ana ninii . . . ana u—uvimbe kwenye ubongo. Si lolote la hayo. [Dada huyo anasema, "Loo, ni kitu gani?"—Mh.] Mshtuko wa mishipa. Yesu Kristo anaweza kumponya mtoto wako mchanga. Unaamini hilo? ["Bila shaka ninaamini."]

Inamisheni vichwa vyenu na kujiunga katika maombi.

42 Mwenyezi Mungu, Yeye aliyemleta Yesu Kristo kutoka kwa wafu, maskini mtoto huyu mchanga asiye na hatia, aliyeketi hapa kwenye mkono wa mama yake, mtoto mdogo mzuri wa kupendeza, maisha yake yataangamizwa kabisa kama Wewe hutaingilia na kusaidia. Madaktari Wako wamefanya yote ambayo wao . . . Umewapa maarifa ya kufanya; lakini huyu mama ameniletea mtoto huyu mchanga ili nipate kukuomba Wewe umsaidie. Na Ee Mungu, kwa uaminifu na unyofu wa moyo wangu, ninaomba nipate rehema. Ee, Wewe uliyemfufua Kristo katika wafu (na wakati alipokufa kule Kalvari, iliangamiza enzi na kumpokonya ibilisi kila mamlaka aliyokuwa nayo), ninasimama mahali Pake usiku wa leo, kama mtumishi Wake, nami ninamkemea ibilisi ambaye ameyafunga maisha ya mtoto huyu mchanga, na jalia amwache, na mtoto apone na awe mzima. Katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ninaomba hili. Amina.

43 Vema, mama, mpeleke mtoto wako nyumbani nami . . . hakika tu kadiri ninavyoamini nimesimama jukwaani, mtoto wako atapona na kuwa mzima. Mungu ambariki. Ubarikiwe. Mungu akubariki, dada.

Hebu tuseme, "Mungu ashukuriwe, Yeye atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo."

44 Unataka kuondokana na ugonjwa huo wa tumbo, uliyeketi hapo ukiomba, dada? Uliyeketi moja kwa moja hapo chini, unataka kuondokana nao? Mama aliyeketi karibu nawe, mwenye ugonjwa wa mgongo hapo, unataka kuondokana nao? Nyote

wawili? Mnaamini? Vema, simama tu na kulikubali. Mungu atakuponya. Amini kwa moyo wako wote. Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yuko hapa kukuponya. Ugonjwa wa wasiwasi husababisha kidonda cha tumbo. Imani yako inathibitishwa nao, inakufanya mzima. Jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuamini.

45 Wewe huko juu uliyevaa ninii ya manjano, huko juu kwenye kusa-. . .huko juu kwenye roshani ukiomba, unataka Mungu akuponye, jambo pekee likupasalo kufanya ni kuinua mkono wako. Si lazima uwe na kadi ya maombi. Huna kadi ya maombi, sivyo, mama? Bila shaka huna. Yeye haninii. . .Si lazima uwe na kadi ya maombi. Kitu pekee unachopaswa kuwa nacho ni imani. Amina. Loo, jinsi angetandaza mbawa Zake kuu hapa na kumponya kila mtu hapa ndani, ikiwa tu utamruhusu. Ungetaka kufanya nini cha ziada?

46 Musa alipokutana na Wamisri, ama, alipokutana na Waisraeli, hakuweka mkono wake kifuani mwake, kuthibitisha kila wakati alipomwona Mwisraeli. Alifanya hivyo wakati mmoja, nao Israeli wote wakamwamini.

47 Na kama mnaamini yale ninayowaambia kwamba ni kweli, kisha Mungu anayathibitisha kwamba ni kweli, kisayansi na kiroho pia, aminini jambo hili, ya kwamba ninawaambia ukweli: kwamba Yesu alimponya kila mmoja wenu miaka elfu moja mia tisa iliyopita wakati alipokufa kwa ajili yenu; na jambo pekee likupasalo kufanya ni kulikubali sasa hivi na uponywe, haidhuru ugonjwa wako ni upi. Hizi ni ishara tu na maajabu kuthibitisha ya kwamba Yeye anawapenda, na upendo Wake upo hapa kwa ajili yenu.

48 U hali gani, mama? (Huyu ndiye mgonjwa, Ndugu Bosworth? Huyu ndiye mgonjwa? Huh?) Njoo hapa. Samahani, maono wakati mwingine huniondokea na mimi—mimi huwa dhaifu sana kutokana na kuzungumza sana, nayo huniacha. Maikrofoni hii ni hai; hiyo ndiyo sababu ninakaa hapa juu.

49 Ninakutaka uniangalie kwa dakika moja tu. Sijawahi kukuona maishani mwangu, nijuavyo mimi. Hatufahamiani kabisa. Sijui lolote kukuhusu, bali Mungu anakujua. Huyu hapa mwanamke ambaye sijawahi kumwona maishani mwangu. Mwenyezi Mungu anajua ukweli ni upi. Hatujawahi kukutana hapo kabla maishani mwetu, nijuavyo mimi. Nadhani hatujakutana, sivyo, dada?

50 Kama Mungu atamfunulia mwanamke huyu shida yake ni nini, je, itaithibitisha Biblia na kutimiza Maandiko, ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele?

51 Kadiri ningeweza kuzungumza, dada, bila shaka, ndivyo mengi yangesemwa. Lakini unatambua inadhoofisha tu na kudhoofisha nami nina—nina mstari mrefu sana wa maombi

ulioitishwa, pale juu. Kama atanena tu shida yako, utaamini? Utaamini.

52 Una matatizo matatu. Mojawapo ni ugonjwa wa tumbo, ambao ni uvimbe tumboni. Hiyo ni kweli? Wasiwasi, ugonjwa wa kibofu nyongo, hiyo si ni kweli? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa, kama Mungu amesimama hapa kuthibitisha kweli, nawe unajua hiyo ni kweli. Sivyo? [Huyo dada anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Lakini uchunguzi wako na kila kitu vinathibitisha kwamba ni kweli; daktari wako alisema hivyo; na mambo haya yote yanatangaza ni kweli; na mimi, mgeni, ninakutangazia hilo. Basi nakutangazia, ya kwamba, endapo imani yako inaweza tu kugusa upindo wa vazi Lake kule, ama, kugusa ahadi Yake, ambapo (alipokufa pale Kalvari), kama ungekubali uponyaji wako, hali hiyo ya mwili wako (chochote ilicho, sijui sasa, ila chochote ilichokuwa) itakuacha. Unaamini hilo?

53 Basi nimewaambia ukweli. Ndipo Yesu akasema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya." Hiyo ni kweli?

54 Mwenyezi Mungu, kuthibitisha Neno Lako, kama mtumishi mwaminifu, ninaweka mikono yangu juu ya mwanamke huyu, katika Jina la Yesu Kristo, na kuomba kwamba ugonjwa wa mwili wake umwondokee, wala usimsumbue tena. Amina.

Sasa, nenda ukiamini, dada. Nenda ukishangilia, nenda ukifurahi, nenda ukimwambia kila mtu kuhusu uponyaji wako. Uh-huh.

55 Vema, njoo mama. Unaamini kwa moyo wako wote? Je, ungependa kuondokana na hicho kisukari? Sema, "Ninaukubali uponyaji wangu." [Huyo dada anasema, "Ninaukubali uponyaji wangu."—Mh.] Mungu akubariki. Hivyo tu ndivyo unavyoweza kufanya, dada. Nenda useme, "Asante, Bwana Yesu," na uponywe. ["Asante, Yesu."] Amina. Mungu akubariki.

56 Vema, njoo kwangu. Hivi unaamini, mama, unapokuja? Unaamini. Kama Mungu anakujua, Yeye anajua shida yako. Hiyo ni kweli? Wewe ni Mkristo, mwaminio. Maisha hayajakuwa kitu rahisi kwako. Umekuwa na mapito mabaya, ya kuhuzunisha, magumu sana. Hiyo si ni kweli? Ninaona mchirizi mweusi; ukishuka chini yake. Unaugua sasa ugonjwa wa moyo. Na kilichousababisha ni moyo wenye wasiwasi. Umekuwa na wasiwasi kwa muda mrefu, tezi, na kila kitu upande wa ndani. Mungu anakuponya sasa. Unaamini hilo?

Katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, jalia apokee uponyaji wake. Amina.

Sasa, nenda ukimshukuru Mungu. Usiushuhudie tena, utapona.

Hebu tuseme, "Mungu na ashukuriwe."

57 Njoo, ndugu yangu. Ninakutaka, uweke tu mkono wako begani mwangu hapa, bwana. Ikiwa Mungu, bila kukuangalia, atanionyesha, huko nje, shida yako...Maana nilihisi mvuto fulani, ukaja ufahamu: kasema nilikuwa “nasoma akili.” Sikujui, lakini kama Mungu, hapa nje, atashuhudia katika ono, huko nje mbele yangu, hapa, shida yako, je, utaukubali uponyaji wako? Kama utaukubali, tikisa kichwa chako. Utaukubali.

58 Umefanyiwa uchunguzi, una wasiwasi, una ugonjwa wa tezi dume, na unasumbuliwa na ugonjwa wa moyo. Hiyo ni kweli? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Haya basi. Vema, nenda zako, upate afya, katika Jina la Bwana Yesu.

59 Njoo, mama. Loo, Kanisa la Mungu aliye hai, tunawezaje kukaa kimya? Kama mnaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake, kwenye kusanyiko hili sasa hivi, sijui kama ni mimi, lakini inaonekana tu kwangu kana kwamba ni kusanyiko lote, huko nje, linakuwa tu kama krimu, maziwamaziwa tu. Roho Mtakatifu yuko karibu, enyi marafiki. Inaonekana tu kana kwamba ni—ni kama tu kusukuma; chochote kingeweza kutokea.

60 Mama, unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini ya kwamba Mungu yuko hapa kukuponya? Kama nitafanya hivyo, kwa Roho wa Mungu, kwa nguvu za upambanuzi, kupita kivuli chochote cha shaka (nawe utajua kama ni kweli au la), kwa msaada wa Mungu, kukwambia shida yako ilipo, kulingana na yale Yesu Kristo alisema ya kwamba angefanya katika siku hizi za mwisho, utamkubali Yeye kama Mponyaji wako? Una ugonjwa wa tumbo. Hiyo ni kweli? Kama ndivyo, punga mkono wako namna hiyo. Sasa, nenda ule utakacho. Mshukuru Mungu kwa moyo wako wote.

61 Njoo, mama. Sasa, unapokuja, ninataka uamini. Ninataka, kuushika mkono wako. Hivi unaamini ya kwamba nguvu za Mungu zilizomfufua Kristo katika wafu zimesimama hapa na zinajua mambo yote? Wewe na yule mama aliyeketi pale nyote wawili mna ugonjwa wa figo. Nyote wawili mmeponywa sasa, mnaweza kwenda nyumbani na kuwa wazima. Mungu awabariki. Nendeni tu mkishangilia. Mungu akubariki, dada, na ujaliwe.

62 Njoo, mama. Utaamini kwa moyo wako wote? Unataka kuondokana na ugonjwa huo wa mgongo ulio nao? Vema, endelea tu kumshukuru Mungu, na kusema, “Imekwisha katika Jina la Bwana Yesu.”

63 Njoo, mama. Unaamini kwa moyo wako wote? Una tatizo kwenye mguu wako, sivyo, mama? Naam. Unataka kuponywa? Vema, simama kwa miguu yako na ukubali uponyaji wako katika Jina la Bwana Yesu. Amina. Mungu akubariki.

64 Weka mkono wako juu ya mume wako hapo, aliyeketi karibu nawe, akiwa na ugonjwa wa kibofu nyongo, na aponywe pia.

Mungu akubariki. Endelea, nenda nyumbani na ule unachotaka, shida yako ya tumbo imekuondokea, mama. Unaweza tu kwenda na kula chochote utakacho.

Hebu tuseme, "Mungu na ashukuriwe."

Ndugu, unaamini ugonjwa wako wa moyo ulikuacha ulipokuwa umeketi pale? Nenda ukimshukuru Mungu, na uwe mzima kabisa. Amina.

65 Njoo, mama. Usiketi chini, njoo tu huku. Unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini kwamba pumu ilikuacha ulipokuwa umeketi pale? Toka tu jukwaani ukipaza sauti na kumsifu Mungu, na kumshukuru Mungu kwa wema Wake.

Nenda, ndugu yangu, ukimshukuru tu na kumsifu Mungu kwa ajili ya wema Wake; na Mungu wa Mbinguni akubariki.

Hebu tuseme, "Mungu na ashukuriwe."

Nini . . . Loo, ndugu, dada, kwa nini tunakuwa tumekufa ganzi sana rohoni mwetu?

66 Jinsi Mungu wa Mbinguni alivyomfufua Mwanawe, Kristo Yesu, Ambaye anaonekana sasa, kumponya kila mtu. Mlete huyo mtu. Yeye anazungumza naye, ama kitu fulani, hebu kidogo.

67 Wakati anapofanya hivyo, nashangaa, ni wangapi hapa ndani ambao kweli wanatamani sana kuponywa? Inua mkono wako. Mnaamini nimewaambia kweli? Mnaamini ya kwamba Mungu amelithibitisha kisayansi? Mnaamini ya kwamba Mungu amelithibitisha kwa Neno Lake? Mnaamini ya kwamba Mungu amelithibitisha kwa Roho Wake? Basi, katika kinywa cha mashahidi watatu kila Neno na lithibitishwe.

68 Kila mwanamume na mwanamke hapa ndani anayetamani kuponywa, na ainamishe kichwa chake sasa hivi, na uombe dua kwa Mungu kwa ajili ya uponyaji wako. Nitawaombea. Billy, weka tu mkono wako juu ya mwanamke huyo papo hapo mahali anaposimama. Inamisheni vichwa vyenu, kila mahali.

69 Bwana Yesu, ninaomba ya kwamba utawarehemu, sasa hivi, maskini watu hawa, wahitaji, wanaoteseka. Wakati nguvu za mwili wa mtumishi Wako zikiisha, ninaomba ya kwamba utanirehemu, Mungu, na utamtuma Roho Mtakatifu, sasa hivi. Na jalia watu, tuseme, wazichune roho zao kwa Neno la Mungu, na kuamka na kutambua ya kwamba hii ndiyo saa ya kutembelewa kwa Owensboro, Kentucky, wakati Roho Mtakatifu anapotenda kazi miongoni mwa watu, na kuonyesha ishara na maajabu. Ee Mungu wa Milele, mtume Roho Wako Mtakatifu, na umponye kila mmoja wao, katika ninii la Yesu Kristo . . .

53-1107 Yesu Kristo Yeye Yule
Jana, Leo, Na Hata Milele
Sportscenter
Owensboro, Kentucky Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org